


**Learning on TAP**

# Teknolojia saidizi
## Maneno muhimu: Vifaa saidizi vya usikivu vinavyoweza kusetiwa

| **Neno** | **Maana** | **Picha** |
|---|---|---|
| **Apu** | Kifupisho cha neno linalomaanisha programu. Ni kifaa cha kidigitali kinachotumika kwenye simu au kishikwambi kufanya kazi maalumu. | |
| **Odiogramu** | Ni chati ya usikivu wa mhusika anayepimwa inaonyesha sauti ya chini kabisa ambayo mhusika anaweza kusikia (kiwango cha mwisho cha sauti) katika mafasa tofauti ya sauti. |  |
| **Odiomita** | Kifaa cha kupima usikivu |  Apu ya odiomita iliyo kwenye kishikwambi |
| **Wastani wa kiwango cha sauti cha chini kabisa ambacho mhusika anaweza kusikia** | Hesabu ya kujumlisha viwango vya sauti vya chini kabisa ambavyo mhusika anayepimwa anaweza kusikia vya 500 Hz, 1000 Hz, 2000 Hz, na 4000 Hz halafu kugawa idadi kwa nne. | |
| **Mtaalamu wa masikio na usikivu** | Wataalamu ambao hupima, husimamia na kutibu matatizo ya masikio na usikivu. | |
| **Mwangwi** (Mluzi) | Sauti ya "filimbi" kutoka kwenye kifaa saidizi cha usikivu pale ambapo sauti inapenyeza kutoka kwenye sikio na kupokelewa na kipaza sauti cha kifaa saidizi cha usikivu. | |
| **Masafa** | Ni mara ngapi  mawimbi ya sauti yanasafiri juu na hcini ndani ya sekunde moja. Kuna aina tofauti za sauti ikiwepo sauti nzito ( masafa ya chini) kama vile sauti ya ngoma na vitu vilivyonolewa (masafa ya juu) kwa mfano filimbi. Masafa yanapimwa kwa Hezi (Hz) |  |
| **Sauti ya chini kabisa ambayo inaweza kusikika** | Sauti ya chini kabisa ambayo mgonjwa anaweza kusikia katika masafa tofauti ya sauti. | |
| **Hezi** (Hz) | Namna ya kupima idadi ya mara ngapi kitu kinatokea ndani ya sekunde moja. Kwa mfano, kama mawimbi ya sauti yanatetemeka mara 100 ndani ya sekunde moja, yana masafa ya Hz 100. | |

| | | |
|---|---|---|
| **Sauti za Lingi** | Seti ya sauti sita.<br>Sauti hizi huchukua wigo wote wa sauti za maongezi kwa masafa ya chini hadi masafa ya juu |  |
| **Fomula ya kuweka kiwango sahihi cha usaidizi wa usikivu kulingana na upungufu wa kusikia** | Mahesabu ya kiwango cha sauti kinachoongezeka kwa kila masafa kulingana na matokeo ya kipimo cha usikivu. | |
| **Kifinyazi cha sikio kilichotengenezwa kwa ukubwa uliozoeleka** | Sehemu ya kifaa saidizi cha usikivu ambayo imetengenezwa tayari katika ukubwa tofauti ili kuweza kutosha kwenye sikio la mhusika. Inaunganisha na kifaa saidizi cha kusika kwa kutumia bomba na hufikisha sauti kwenye sikio la mtumiaji. |  |
| **Stetoklipu**<br>(Bomba la kusikiliza) | Inajulikana vilevile kama bomba la kusikiliza. Linamruhusu mtumiaji mwenye usikivu wa kawaida kufuatilia kujua kama kifaa saidizi kinafanya kazi vizuri. |  |